# HABARI PICHA




MAKAMU wa Rais Dk. Philip Mpango, akipata maelezo kutoka kwa Wakili wa Serikali Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Elia Athanas (kulia) alipotembelea banda la wizara hiyo katika Maonyesho ya Wiki ya Sheria, Dodoma, jana. Kushoto ni Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma na wa pili kulia, Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Khatibu Kazungu. (Na Mpigapicha Wetu).

**Habari leo 24/01/ Uk. 18**

# Changamkieni elimu bure Wiki ya Sheria-DC

Na Happiness Katabazi, Liwale

MKUU wa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Judith Nguli amewataka wananchi kwenda kupata elimu bure ya sheria katika maeneo yaliyotengwa na Mahakama ili iweze kuwasaidia katika maisha yao ya kila siku.

Hayo aliyasema jana katika uzinduzi wa wiki ya sheria ambayo kilele chake ni Januari 29 iliyofanyika katika Mahakama ya Wilaya ya Liwale iliyopo eneo la Mokonji Ganga. Uzinduzi uliambatana na matembezi yaliyoanzia Lena Elimu.

"Nawashauri nendeni katika hayo maeneo yaliyotengwa na Mahakama mkapate elimu ya sheria na miongozo bure ili mpate elimu ya kutatua migogoro yenu kwa amani bila kwenda mahakamani…ikumbukwe kuwa jamii yenye migogoro haiwezi kukua kiuchumi wala kupata maendeleo," alisema Nguli.

Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Liwale, Nico Mwakibibi alisema katika kuadhimisha wiki ya sheria wametenga maeneo matano ambayo amewataka wananchi wafike wakapate elimu ya sheria iwasaidie kuwa na uelewa wa masuala ya sheria katika maisha yao.

Hakimu Mwakibibi alisema wamezindua dawati la sheria ambalo lipo ndani ya mahakama hiyo. Pia watakwenda gereza la Wilaya Liwale, Soko la Zain na Kituo Kikuu cha mabasi wilayani hapo. Pia mahakama imewaalika viongozi wa vyama vya ushirika wafike mahakamani hapo ili waweze kupewa elimu.

Aidha, alisema uzinduzi wa mwaka mpya wa mahakama utafanyika Februari Mosi, mwaka huu, katika viwanja vya Mahakama ya Wilaya na kaulimbiu ya mwaka huu ni umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu.

Dailynews 25/01/2023 uk. 4

# Prof Gabriel hails President Samia on court infrastructures improvement

From PILLY NASHON in Dodoma

THE Chief Court Administrator, Professor Elisante Ole Gabriel has commended President Samia Suluhu Hassan for endorsing funds for improving, renovating and building court infrastructures countrywide.

Prof Gabriel issued the compliments here on Monday when he visited the ongoing law week exhibition held nationally at Nyerere Grounds. He said that through the concessional loans given by the World Bank (WB), the Sixth Phase Government has provided 207bn/- for increasing scope of access to justice for the people.

"I sincerely thank the sixth phase government under the leadership of President Samia because it allocates a lot of money to make court infrastructures friendly. The funds are well spent and that the results are seen.

"Court infrastructures improvement depends on the government's facilitation, in fact, we are well empowered. Through the WB we have received 207bn/- for improving the infrastructure of our courts in the country," said Prof Gabriel, adding that without the government's efforts there would be a big challenge.

He noted that with government's efforts, construction of primary courts, the resident magistrate's courts and High Court is going on at a fast pace. He stated that already six integrated centres have been built in five regions and nine others will be built by 2024.

"The aim of building the integrated centres is not just to have the buildings, but to ensure that justice delivery is improved. Citizens need to create a culture of monitoring the work done by the courts because the government has made significant improvements," said Prof Gabriel.

Explaining on the unethical conducts by some of the court officials, he said the issue should not discourage Tanzanians in seeking justice from the court as an institution.

"The court does not do business, it provides services. Judgments are not made arbitrarily, they are based on national laws, so people need to continue to believe in the judiciary staff that they are doing justice and if some court officials act unethically there are appropriate systems to follow to correct each other," he said.

The Deputy Secretary of the Court Service Commission, Enziel Mtei, said currently issues related to services by court employees are handled by the Commission, whose members and subordinates are specified in the Constitution and the law on court operations.

He said the Court Operation Law directs to have Judges ethical committees in regional and district levels whose job is to investigate complaints against judges and other lower level court administrators.

"We are here to educate the public and we will continue to provide it to ensure that citizens understand the services provided by this Commission and how they can submit their complaints to regional and district moral committee," she said.

Majira 25/01/2023 uk. 8

# Ataka wananchi waiamini mahakama utendaji haki



MTENDAJI Mkuu wa Mahakama, Profesa Elisante Ole Gabriel amewataka wananchi kuendelea kuuamini mhimili wa mahakama kwani unatenda haki.

Profesa Gabriel alisema hayo jijini hapa jana alipotembelea Maonesho ya Wiki ya Sheria ambayo kitaifa yanafanyika katika viwanja vya Nyerere Square.

Aliwataka wananchi kuendelea kuuamini mhimili wa mahakama kwani unatenda haki na pale ambapo kunaweza kuwa na shaka yoyote kwa baadhi ya watumishi ambao pia ni binadamu kuna na mifumo mizuri ya kurekebishana.

"Tuna mifumo mizuri ya kurekebishana, nadhani hilo lisihamishe imani ya Watanzania kwa mhimili wa mahakama, ndani ya mahakama kuna miongozo mizuri na sheria zitafuatwa. Maamuzi ya kisheria hayafanyiki kiholela yanazingatia sheria hivyo wananchi wanatakiwa kuendelea kuwa unatenda haki," alisema.

Aidha, amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha, kukarabati na kujenga miundombinu ya mahakama.

Alisema kupitia mkopo wa masharti nafuu uliotolewa na Benki ya Dunia, awamu ya pili serikali imeipatia mahakama Sh bilioni 207 kwa ajili ya kuongeza wigo wa upatikanaji haki kwa wananchi.

"Natoa shukrani za dhati kwa serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa sababu inatoa fedha nyingi kwa ajili ya kuiwezesha mahakama kuwa na miundombinu rafiki na fedha inatumika vizuri ambapo matokeo yameanza kuonekana.

Alisema: "Utoaji haki hatuuzi, miundombinu yetu inategemea sana uwezeshaji wa serikali. Kwa kweli, tunawezeshwa vizuri. Kupitia fedha za WB tumepokea Sh miundombinu ya mahakama zetu nchini.

Profesa Gabriel alisema bila uwezeshaji wa serikali, kungekuwa na changamoto kubwa ya kimiundombinu ambapo kwa sasa ujenzi wa mahakama za mwanzo, hakimu mkazi na mahakama kuu zinaendelea kwa kasi kubwa.

Alisema wameshajenga vituo jumuishi sita katika mikoa mitano na vingine tisa vitajengwa ifikapo mwaka 2024.

"Lengo la kujenga vituo hivyo sio kuwa na majengo bali ni kuhakikisha miundombinu ya utoaji haki inaboreshwa.

"Wananchi wanatakiwa kujenga utamaduni wa kufuatilia kazi zinazofanywa na mahakama kwani serikali imebadilisha," alisema.

Naye, Naibu Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Enziel Mtei alisema kwa sasa masuala yote ya utumishi kwa watumishi wa mahakama yanashughulikiwa na tume hiyo yake yameainishwa katika katiba na sheria ya uendeshaji wa mahakama.

Alisema sheria ya uendeshaji wa mahakama inaelekeza kuhusu kuwepo kwa kamati za maadili ya mahakimu katika ngazi za mikoa na wilaya ambazo kazi yake ni kuchunguza malalamiko dhidi ya mahakimu.

"Katika kutekeleza majukumu yake, tume ya utumishi wa mahakama inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo baadhi ya wananchi kutofahamu vyema kuhusu majukumu yake na kamati zake.

"Pia wananchi wenye malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa maadili ya maofisa wa mahakama kutojua utaratibu na sehemu sahihi ya kuwasilisha malalamiko yao," alisema.

"Ili wananchi waweze kufaidika na huduma zinazotolewa na tume hiyo, hawana budi kuelewa kazi za tume na umuhimu wake katika kusimamia utumishi wa mahakama ya Tanzania," aliongeza.

Uhuru 25/01/2023 uk. 4

# HOJA YA HAJA

> Siandiki haya kuzuia kesi kufunguliwa mahakamani, bali nashauri kwa nia njema ya kumaliza milolongo ya mashauri mahakamani ambayo...



Na HEMED MUNGA, OUT

# Wadau wa sheria, viongozi wa dini waelimishe jamii faida za usuluhishi

MATUKIO ya migororo mbalimbali katika jamii inatoa taswira kwa wadau wa sheria na viongozi wa dini kwamba bado wana jukumu la kutoa elimu kuhusu namna ya kupata haki kwa njia sahihi.

Hivi sasa kumekuwa na wimbi la migogoro itokanayo na ardhi, talaka, mirathi, unyanyasaji wa kijinsia, hivyo kuifanya jamii kupoteza muda kwa kushughulikia migogoro badala ya kujikita katika shughuli za kukuza uchumi.

> **Hata hivyo, naamini huu ni wakati wa wadau wa sheria na viongozi wa dini, kushauri umuhimu wa upatanishi na kujenga jamii yenye maridhiano.**

Uimara wa taifa lolote katika nyanja mbalimbali unatokana na watu wake kudumu katika shughuli za uzalishaji.

Nashauri kila mtu aone umuhimu wa kuepuka migororo, hasa katika kipindi hiki cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ambacho ni rahisi sana kufikisha elimu kwa jamii.

Hata hivyo, naamini huu ni wakati wa wadau wa sheria na viongozi wa dini, kushauri umuhimu wa upatanishi na kujenga jamii yenye maridhiano.

Jamii ikielimika itakuwa na uwezo wa kujilinda na kuepuka migogoro katika maeneo yao.

Natoa hoja hii zikiwa zimepita siku chache tangu kufanyika uzinduzi wa Wiki ya Sheria nchini, ambapo aliyekuwa mgeni rasmi Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, aliwaasa viongozi wa dini na kimila kuisaidia mahakama kuzungumza na wananchi kuhusu umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi.

Kauli hiyo ya Dk. Mpango, inadhihirisha jamii haina elimu ya kutosha ya namna ya kufikisha migogoro katika vyombo vya sheria na kupata haki zao.

Hivyo, ni vizuri wadau wa sheria kutumia ubunifu na njia mbalimbali za mawasiliano, kufikisha elimu hususan kwa jamii ya vijijini na mijini, kutambua madhara ya migogoro na namna ya kuitatua kwa usuluhishi.

Nashauri siyo lazima kumaliza mgogoro kwa kuufikisha mahakamani ambako huchukua muda mrefu kumalizika, badala yake usuluhishi au upatanishi ufanyike sehemu nyingine ili kufikia maridhiano.

Siandiki haya kuzuia kesi kufunguliwa mahakamani, bali nashauri kwa nia njema ya kumaliza milolongo ya mashauri mahakamani, ambayo yamekuwa yakisababisha ucheleweshaji wa haki na wakati mwingine machafuko kushika kasi katika jamii.

Pande zinazovutana zikipata suluhu nje ya mahakama hakika amani, upendo, umoja na mshikamano huwa zinaifanya jamii kusikilizana na kujikuta wakiwa wamoja katika kuchochea shughuli za maendeleo.

Nipashe 24/01/2023 uk. 16

# DC afichua mbinu mpya ya mahakimu kupokea rushwa

Na Nebart Msokwa, MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, amesema baadhi ya mahakimu na majaji mkoani Mbeya wamebuni mbinu mpya ya kupokea rushwa kwa kutumia miamala ya simu zisizokuwa zao ili kuficha utambulisho wao pale wanafuatiliwa na vyombo vya dola.

Alifichua mbinu hiyo wakati wa maadhimisho ya Wiki ya Sheria nchini, ambayo kimkoa yalifanyika katika viwanja vya Kabwe jijini Mbeya.

Dk. Chuachua alisema amepokea malalamiko mengi ya wananchi wakiwalalamikia baadhi ya mahakimu na majaji kwa vitendo vya rushwa.

Alisema kila akifuatilia malalamiko hayo ya wananchi hubaini kuwa watumishi hao wa mahakama hupokea rushwa hiyo kwa miamala ya simu zisizokuwa za kwao ili wasibainike.

"Changamoto kubwa tuliyonayo ni kwamba hatuna mamlaka ya kuingilia mfumo wa mahakama, lakini niseme tu hapa, kwamba upo utaratibu wa mahakimu kuomba rushwa kwa kutoa namba za miamala ya simu zisizo zao, sio rahisi kuwakamata kwa kutumia miamala ya simu," alisema Dk. Chuachua.

Alisema kuwa wananchi wamefika kulalamika wakiwa tayari wametoa fedha kupitia miamala ya simu, lakini unapofuatilia miamala hiyo unakuta simu hizo sio za mahakimu.

Aliitaka Mahakama ya Tanzania kufuatilia na kukomesha vitendo hivyo miongoni mwa watumishi wa mahakama ili kuhakikisha wananchi wanapata haki wanazostahili.

Akizungumzia mbinu hiyo, Naibu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, Valsela Malimoto, alikemea vitendo hivyo kwa kusema kuwa vitendo hivyo ni kinyume cha sheria na kwamba taasisi hiyo inao uwezo wa kufuatilia na kuvikomesha.

Alisema kuwa endapo hakimu au jaji atathibitika kufanya vitendo hivyo atakuwa pia amefanya kosa lingine la uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Rose Ebrahim, alisema kuwa Mahakama inachukua kero hiyo na inakwenda kufanyiwa kazi.

Alisema kuwa kupitia vikao vyao vya ndani watachunguzana, kukemeana na ikiwezekana kuwajibishana pale watakapobaini kuwa miongoni mwao kuna watumishi wanafanya vitendo hivyo.

Baadhi ya wadau wa sheria walisema kauli mbiu ya wiki ya sheria mwaka huu, inayosema 'Umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu ni nzuri na imekuja katika muda mwafaka.

Hata hivyo Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu iliomba TAKUKURU kufanya uchunguzi wa tuhuma hizo za rushwa zilizoibuliwa ili hatua zichukuliwe endapo itathibitika kuwa ni kweli.

Habari Leo 24/01/2023 uk. 18

# 'Usuluhishi ni njia bora ya utatuzi wa migogoro'

**Na Swaum Katambo, Mpanda**

WANANCHI wengi wanadaiwa kutopenda njia ya usuluhishi kwa kuamini kuwa kazi ya mahakama ni moja, ya kufunga watu gerezani.

Hayo yalibainishwa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi Mahakama ya Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Glory Mwakihaba katika uzinduzi wa wiki ya Sheria uliofanyika kiwilaya katika viwanja vya Shule ya Msingi Mpanda Ndogo Kijiji cha Majalila Kata ya Tongwe.

Mwakihaba alitumia fursa ya maadhimisho hayo kuwaelimisha wananchi kwamba usuluhishi ni njia bora na rahisi katika utatuzi wa migogoro, inayotumika duniani kote ukilinganisha na uendeshaji wa kesi kwa njia ya kawaida.

Alisema kesi huchelewa kukamilika na kuchukua muda mrefu kwa sababu ya kufuata sheria na taratibu kitendo ambacho kinadumaza uchumi wa mtu mmoja na Taifa kwa ujumla.

"Mwananchi atapoteza muda wake mwingi kuhudhuria mahakamani na kukosa muda wa kufanya shughuli za uzalishaji," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa katika wilaya hiyo, kwa muda mfupi waliofanya kazi wamebaini kuwa vitendo vya kujichukulia sheria mkononi, matukio ya ukatili wa kijinsia, mauaji zikiwamo mimba za utotoni ni matukio yanayoongoza kujirudia mara kwa mara hivyo watajikita katika kutoa elimu zaidi kwa wananchi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Onesmo Buswelu, alitoa wito kwa taasisi zote za serikali kutoa ushirikiano wa kutosha ili mhimili wa Mahakama utekeleze na kufikia azma ya kutoa elimu kwa wananchi.

"Wananchi hawa ninyi mnafanya nao kazi, lakini wakati huo wakiwa wamesongwa na migogoro inayowezekana katika nafasi zenu na majukumu yenu hamjafanikiwa kuitatua, lakini kupitia elimu ambayo mahakama itatoa kwa muda wa juma zima tutapata elimu ya kutusaidia," alisema Buswelu.

Baadhi ya wananchi, walisema watatumia fursa ya elimu watakayopatiwa na watendaji wa mahakama wa wilaya, kupunguza matukio yanayovunja sheria za nchi yanayoweza kuepukika katika jamii.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni: Umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu; wajibu wa Mahakama na wadau.

Kauli hiyo imebeba ujumbe muhimu kuhusu wajibu wa mhimili huo wadau kutumia njia ya usuluhishi kutatua migogoro kwa lengo la kukuza uchumi endelevu.

Habari leo 23/01/2023 uk. 6

# Wiki ya Sheria ni fursa, umma uchangamkie

MAADHIMISHO ya Wiki ya Sheria nchini yamezinduliwa jijini Dodoma mgeni rasmi akiwa Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo jana, Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma alisema yanakwenda hadi Januari 29 kabla ya Februari Mosi, ambayo ndiyo Siku ya Sheria itakayoadhimishwa jijini humo.

Kaulimbiu ya Wiki ya Sheria mwaka huu inasema, **'Umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu, wajibu wa mahakama na wadau.'**

Miongoni mwa shughuli zilizotajwa kuwa zitafanyika katika wiki hii ya sheria inayoadhimishwa kote nchini ni kutoa elimu ya sheria kwa umma, kusikia vipindi vya redio na runinga, maonesho, midahalo maalumu inayohusu usuluhishi.

Pia kutakuwa na uzinduzi wa kitabu cha miaka saba cha Kituo cha Usuluhishi na uzinduzi wa majengo manne ya mahakama ya wilaya utakaofanywa na Jaji Kiongozi katika mahakama za Wilaya ya Manyoni, Bunda, Rungwe na Sikonge.

Kama ilivyo kawaida, kupitia maadhimisho haya ambayo huenda sanjari na maonesho, umma hupata fursa ya kufahamu mambo mbalimbali ikiwamo mafanikio na changamoto ndani ya mhimili wa Mahakama na sekta nzima ya sheria.

Rai yetu kwa wananchi ni kutumia fursa hii ya Wiki ya Sheria kupata elimu na huduma za kisheria kwa urahisi na bila malipo.

Ipo hulka iliyojengeka katika jamii kuona shughuli kama hizi ni za kundi fulani la watu, ikadhaniwa maonesho haya ni ya watu wa kada fulani hivyo baadhi ya watu, mfano wasio watumishi, viongozi na watendaji wa serikali wakajiona hayawahusu.

Tunahimiza umma wa Watanzania kuchangamkia fursa hii tukiamini kuwa maonesho yatawawezesha kuelimishwa kuhusu masuala ya kisheria na namna ya kushughulikia malalamiko.

Kupitia Wiki ya Sheria ni rahisi pia kwa wananchi kutoa mapendekezo kuhusu namna bora ya kuboresha shughuli za mahakama na sekta nzima ya sheria kupitia wataalamu na wabobezi wa sheria kutoka sekta ya umma na binafsi.

Tunasisitiza kuwa hii ni fursa adhimu ya kukutana au kusikia wadau wa masuala ya sheria wakielimisha kuhusu mambo mbalimbali ikiwa ni sehemu ya maadhimisho haya yanayofanyika katika kanda za Mahakama Kuu, mikoa na wilaya nchini.

Hata Makamu wa Rais, Dk Mpango amesisitiza kuwa Wiki ya Sheria ni muhimu kwa wananchi kupata msaada wa kisheria na kuelewa shughuli za mahakama, hivyo elimu inayotolewa itasaidia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu huduma za mahakama na utaratibu wa sheria kwa ujumla.

Uhuru 24/01/2023 uk. 6

# Wiki ya Sheria itumike kuwaelimisha wananchi

JUZI Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, alizindua rasmi Wiki ya Sheria iliyokwenda sanjari na matembezi ya hisani ya kilometa tano yaliyoanzia Mahakama Kuu ya Tanzania hadi Viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma.

Mbali ya Makamu wa Rais Dk. Mpango, viongozi wa kada mbalimbali na wananchi walijitokeza kwa wingi kuunga mkono matembezi hayo yenye lengo la kutoa elimu ya sheria.

Aidha, katika maeneo mengine nchini majaji wafawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, walishiriki katika wiki hiyo ya sheria kwa kuwashauri Watanzania kujitokeza kupata elimu ya sheria.

Elimu hiyo itatolewa kupitia maonyesho ya wadau wa mahakama waliwemo polisi, magereza na mawakili katika viwanja vilivyoandaliwa kwa maadhimisho hayo.

Wananchi watapata fursa ya kuelimishwa kwa muda wa wiki moja, kabla kuhitimishwa kilele cha Siku ya Sheria, Februari Mosi, mwaka huu, ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Elimu hiyo inatarajiwa kutolewa kwa namna mbalimbali kupitia vipindi vya redio, televisheni, midahalo na maonyesho ya viwanjani kwa kipindi chote cha maadhimisho.

Tunaamini idadi kubwa ya wananchi watajitokeza kushiriki katika wiki ya sheria kwa lengo la kuchangamkia fursa ya kupata elimu itakayotolewa na wataalamu mbalimbali.

Kupitia maonyesho hayo, tuna imani wananchi watapata ufafanuzi wa changamoto mbalimbali za kisheria zinazowakabili katika maeneo ya kazi, biashara, ardhi au mirathi ambayo imekuwa ikisababisha hali ya sintofahamu miongoni mwa jamii.

Pia, watendaji wa mahakama na wadau wao wanapaswa kuyafanyia kazi maagizo ya Makamu wa Rais, Dk. Mpango, ambaye wakati akizindua wiki ya sheria Dodoma, aliagiza iwaelimishe wananchi kuhusu utatuzi wa migogoro hususan kwa njia ya usuluhishi ambayo ina faida nyingi ikiwemo kuokoa muda.

Makamu wa Rais alisisitiza umuhimu wa kuwa na mfumo thabiti wa kutatua migogoro na kuokoa muda unaotumika katika uendeshaji wa kesi kwa njia ya kawaida.

Kama alivyosema Makamu wa Rais kuhusu faida za usuluhishi, nasi tunaungana naye kwa kuhimiza mhimili wa mahakama na wadau wake, kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuridhia kumaliza kesi au migogoro kwa njia hiyo ambayo inarahisisha kupatikana haki kwa wakati.

Tunaamini wananchi na wadau kwa ujumla, watajitokeza kwa wingi katika wiki ya sheria kwa lengo la kujifunza na watakaobahatika kupata elimu hiyo wakawe walimu kwa wengine katika jamii.

Mwananchi 23/01/2023 uk. 3

# Dk Mpango ataja vikwazo 7 wananchi kutafuta haki

Habel Chidawali, Mwananchi
hchidawali@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Makamu wa Rais, Dk Philip Mpango ametaja mambo saba ambayo ni vikwazo kwa wananchi katika kutafuta haki zao mahakamani huku rushwa ikiwa kinara.

Miongoni mwa mambo hayo ni baadhi ya majaji, mahakimu na mawakili kutokuwa waaminifu kwa kudai rushwa, kesi kuendeshwa siku za Jumapili na upotevu wa fedha za kigeni zinazokamatwa kama ushahidi.

Mambo mengine ni gharama kubwa za uendeshaji kesi, hukumu za lugha ya Kiingereza, watu kusota mahabusu muda mrefu na wakati mwingine umbali kutoka walipo wananchi na maeneo wanakopatikana haki za kisheria.

Habari leo 23/01/2023 uk. 6

Dk Mpango alitoa kauli hiyo jana baada ya kupokea matembezi ya uzinduzi wa Wiki ya Sheria ambayo kitaifa yalifanyika jijini Dodoma. Pia, aligusia mambo mengine kuwa yanawahusu polisi na magereza.

Alisema baadhi ya mahakimu, mawakili na majaji si waaminifu, kwani wamekuwa wakidai rushwa kinyume cha viapo vyao na kutokana na hilo wanapindisha haki, ili kumpa mwenye fedha na asiye na fedha ananyimwa.

Alitolea mfano wa minada ya mifugo ambayo hukamatwa maeneo ya hifadhi, lakini mahakama ikitumika kuamuru iachiliwe kwa faini ndogo huku ikileta sintofahamu kuwa mara nyingine kesi hizo zinaendeshwa kwa siku mbili au hata Jumapili.

"Mfano kule Mbeya tumeletewa malalamiko minada hiyo inazuiliwa kwa amri ya mahakama tena wakati mwingine unashtuka kabisa hiyo mahakama imekaa siku ya Jumapili, ambayo si siku ya kazi," alihoji.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, wakati mwingine faini zinazoamuliwa huwa ni ndogo ambazo husababisha mwenye mifugo kuzilipa na baada ya nusu saa wanairudisha mifugo kwenye hifadhi.

Kuhusu fedha za kigeni, alisema kuna malalamiko zinakamatwa fedha mipakani, lakini mwisho wake huwa zinapotea mikononi mwa mahakama.

Makamu wa Rais alitaja malalamiko



"Jambo kubwa ni kutokufanywa uchunguzi kabla ya kuwa mahakimu maana zamani ilikuwa si rahisi mtu apewe nafasi hiyo kama hajapitia mikono ya uchunguzi, leo wanaomba kama wanavyoomba udereva wakati anakwenda kutoa haki, si sawa kabisa."

Wakili Godfrey Wasonga

mengine kuwa ni gharama kubwa za undeshaji wa kesi na kuwalipa mawakili huku hukumu zikiandikwa kwa lugha ya Kiingereza kwamba ni mambo yanayopaswa kuangaliwa.

"Hili la umbali mrefu lazima mlitazame kutoka walipo wananchi hadi mahakamani na suala la mila na desturi potofu ambazo zinakinzana na sheria hasa suala la mirathi na umiliki wa ardhi kwa wanawake na watoto," alisema.

Hata hivyo, alisema changamoto hizo zinaweza kuepukika na kumalizwa akisisitiza suala la utoaji elimu na matumizi ya Tehama kwamba yanaweza kutoa ufumbuzi.

Awali, Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma alisema baadhi ya wananchi hawafahamu namna ya kuzidai haki zao na wengine huamini kuwa kila anayekwenda mahakamani lazima ashinde kesi.

Profesa Juma alisema utatuzi wa migogoro kwa wananchi imekuwa ni changamoto, licha ya kuwa Tanzania inaongozwa kwa misingi ya haki, sheria na kanuni ikiwemo dira ya Taifa ya mwaka 2020 hadi 2025.

"Wiki hii ya sheria inayoanza leo (jana) hadi Januari 29, moja ya majukumu yetu itakuwa ni utoaji wa elimu kuhusu mambo hayo," alisema.

Kwa mujibu wa Jaji Mkuu, kilele cha Siku ya Sheria ni Februari mosi na Rais Samia Suluhu Hassan anatarajia kuwa mgeni rasmi kwenye maadhimisho hayo yatakayofanyika Jijini Dodoma.

**Maoni ya wadau**

Akizungumzia kauli ya Makamu wa Rais, Wakili Godfrey Wasonga alisema ina ukweli mwingi ndani yake kwani baadhi ya mambo hayo hutokea mahakamani.

Wasonga alitaja mambo mawili makubwa yanayochangia suala la rushwa na kupindishwa kwa sheria ni namna ya upatikanaji wa mahakimu [illegible] kufikia ngazi ya majaji.

Uhuru 24/01/2023 uk. 6

Kingine alitaja tamaa ya fedha kwa mawakili wa kujitegemea akisema baadhi wanadiriki kuwashawishi majaji na mahakimu kwa rushwa, ili washinde kesi za wateja wao na kuonekana kama wanaweza zaidi.

Kwa mujibu wa wakili huyo, baadhi ya majaji huteuliwa kama sehemu ya kuwaondoa kazini hasa wale ambao huwa na nafasi za juu, lakini wakitaka kumbadilisha ndiyo wanamteua kuwa jaji na akaomba vyombo vya uchunguzi vifanye kazi kubwa ya kushauri mamlaka za uteuzi huku akisisitiza mafunzo kwa mahakimu.

Hakimu mstaafu, Geodfrey Pius alisema ndani ya mahakama kuna ushawishi mwingi hasa kwenye suala la rushwa, lakini kinachotakiwa ni namna gani hakimu anaweza kushinda ushawishi huo.

Pius alisema maadili na kuzingatia miiko ndio siri ya mafanikio katika kazi ya kutoa haki kwa wengine na ndiyo inafanya wengi wao akiwemo yeye kufanya kazi hadi kustaafu bila tatizo.

Mkazi wa Kijiji cha Chonde Wilaya ya Bahi, Happy Msambili alidai hakuna haki kwa mtu yeyote anayeitafuta kama hana fedha mkononi.

Alieleza kuanzia polisi, mahakamani na magereza kama mmoja kati ya pande mbili zinazozozana hana fedha, ni bora kuamua kuacha kuliko kushindana kwani wasimamia haki huangalia mwenye fedha.

KI YA SHERIA HABARI ZOTE NA FRED ALFRED, DODOMA

## u kuhusu athari za kujichukulia sheria mkononi

# Mwanasheria afichua sababu wananchi kuchukua sheria mkononi

OFISI ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imetaja sababu za wananchi kujichukulia sheria mkononi, ambazo ni ukosefu wa elimu sahihi ya masuala ya kisheria, mmomonyoko wa maadili na unyanyasaji wa kijinsia.

Kauli hiyo ilitolewa jijini hapa, jana na Wakili wa Serikali, Hery Sanga, katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria ambayo kitaifa yanaendelea Viwanja vya Nyerere Square.

"Sababu ya wananchi kuchukua uamuzi wa kujichukulia sheria mkononi inachangiwa na ukosefu wa elimu sahihi na mmomonyoko wa maadili, ambapo watu wanajikita katika matumizi ya dawa za kulevya, ikiwemo bangi, hivyo kujiamini na kusababisha uvunjifu wa sheria," alisema.

Wakili Sanga alitaja sababu nyingine ni unyanyasaji wa kijinsia, ambapo wanaume wengi huwa wanahisi udhaifu kufika katika vyombo vya sheria kutaka msaada.

Aliwataka wanaume kujitokeza katika vyombo vya sheria wanapohisi wameonewa, sheria ifuate mkondo.

"Kama ikitokea mwanaume amesema anapigwa na ikathibitika sheria itafuata mkondo kwa sababu ni msumeno," alisema.

Kwa upande wake, Wakili wa Serikali, Sindeyan Ngaai, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu athari za kujichukulia sheria mkononi maeneo ya mijini na vijijini.

Alisema kutokana na elimu inayoendelea kutolewa, vitendo hivyo vimepungua ikilinganishwa na miaka ya 2015.

"Vitendo vya wananchi kujichukulia sheria mkononi vimepungua sana na hivi sasa tunaendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali kwa wananchi waelewe kuhusu athari kujichukulia sheria mkononi," alisema.

Kwa upande wa wananchi waliofika katika viwanja hivyo kupata elimu ya masuala ya sheria, walliomba serikali kuendelea kuwachukulia hatua watendaji wanaosimamia sheria wanaokiuka maadili.

Mkazi wa Kata ya Makulu, Eliza John alisema kumekuwa na watendaji wa mahakama wasio waaminifu wanatumia mianya ya kujua sheria na kufanya mwenye haki kuikosa na asiye nayo anapewa.

Aliongeza ni vema watu kama hao wanapobainika wachukuliwe hatua za haraka kwa sababu wanaharibu taswira ya mhimili na kufanya watu kupoteza imani na matumaini.

"Watu wengi wanakata tamaa ya kudai haki zao katika vyombo vya kisheria kwa sababu ya ukiukwaji wa maadili unaofanywa na wachache yaani mtu anajua kabisa sina haki, lakini kwa kuwa ana fedha anaweza kukodi mawakili wakamsimamia na kuipata haki asiyostahiri na kufanya wenye haki kuikosa," alisema.

WIKI YA SHERIA




MTENDAJI Mkuu wa Mahakama, Profesa Elisante Ole Gabriel, akizungumza wakati akikagua banda la Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), katika Maonyecho ya Wiki ya Sheria Kitaifa, viwanja vya Nyerere Square, Dodoma, jana. (Picha na Fred Alfred).

Uhuru 24/01/2023 uk. 6

# NEC kuelimisha vijana kuhusu sheria za uchaguzi

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuanza kutoa elimu ya sheria za uchaguzi kwa vijana, kuwasaidia kuelewa kuwa kushindwa na kushinda zote ni haki katika uchaguzi.

Mkurugenzi Msaidizi, Elimu ya Mpiga Kura wa tume hiyo, Monica Mnanka, alisema hayo jijini hapa, jana na kuongeza NEC imepokea kwa mikono miwili ushauri uliotolewa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Profesa Elisante Ole Gabriel.

Profesa Ole Gabriel alitembelea banda la tume hiyo katika maonyesho ya Wiki ya Sheria yanayoendelea Viwanja vya Nyerere Square na kuishauri NEC kuanza kutoa elimu kwa vijana wadogo kuwajengea uelewa wa kwamba katika uchaguzi kushindwa na kushinda yote ni matokeo.

"Kwa nini msianze kutoa elimu kwa vijana wadogo kutambua kuwa kushinda na kushindwa yote ni matokeo ya uchaguzi, tupunguze malalamiko mengi ya watu kuona wameibiwa, wanaoshindwa wengi hawakubali matokeo baada ya uchaguzi, kuna haja ya kuwaelimisha wakue wakiwa wanatambua kuna haki ya kushindwa na kushinda" alisema.

Mnanka alisema Tume inatambua umuhimu wa elimu ya sheria ya uchaguzi kwa vijana wadogo, hivyo itajipanga kuhakikisha inayafanyia kazi mapendekezo hayo.

"Tunatamani vijana hawa wadogo wafahamu haki na wajibu wao wanapokuwa katika vituo vya kupigia kura au kujiandikisha," alisema.

Mnanka aliendelea kusema pamoja na kuupokea ushauri huo, tume inaendelea kutoa elimu ya mpiga kura na sheria za uchaguzi kwa wananchi kuhusu haki na wajibu wao katika michakato ya uchaguzi na namna tume hiyo inavyofanya kazi.

"Tunashukuru na tumeupokea ushauri wa mtendaji mkuu wa mahakama kwa mikono miwili na niseme tutaufanyia kazi maana kutekeleza jambo hilo ni mchakato," alisema.

Aliongeza kuwa: "Hata hivyo hivi sasa tunaendelea na kutoa elimu ya mpigaji kura kwa wananchi kwa kuwaelimisha kuhusu sheria za uchaguzi na haki zao katika masuala ya uchaguzi."

Pia, tume inatoa elimu kwa vyama vya siasa, wadau na taasisi mbalimbali kwa lengo la kuwajengea uelewa wa namna shughuli za uchaguzi zinavyoendeshwa.

Mbali na hilo, tume inatoa elimu kwa vyama vya siasa namna vinavyoshiriki chaguzi na haki na sheria za uchaguzi kuepuka changamoto zinazosababishwa na kutoeleweka.

"Tunatoa elimu na tutaendelea kuitoa kwa wananchi, vyama vya siasa na wadau wote zikiwemo taasisi za kiraia na mashirika ya kimataifa, kuwajengea uwezo na uelewa kuhusu sheria zetu za uchaguzi. Kumekuwa na changamaoto na malalamiko kwamba mbona sisi siyo kama Kenya ambako mtu akishindwa anaenda mahakamani, wakati sheria yetu ya uchaguzi inasema uamuzi wa tume ndiyo wa mwisho," alisema.

Taasisi 34 zinashiriki maonyesho ya Wiki ya Sheria jijini hapa, yatakayofikia tamati Februari Mosi, mwaka huu, wakati wa kilele cha Siku ya Sheria.

**Ushiriki**

**MAONYESHO**

Taasisi 34 zinashiriki maonyesho ya Wiki ya Sheria jijini hapa, yatakayofikia tamati Februari Mosi, mwaka huu, wakati wa kilele cha Siku ya Sheria.



# 'Marufuku kumalizana kienyeji kesi za jinai'

**Na Amina Omari, Tanga**

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba amehadharisha wazazi, walezi na jamii wanaoendelea kumalizana kienyeji na wahalifu wa vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa kwa watoto.

Aliwataka kuacha tabia hiyo kwa kusema serikali itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani wanapobainika.

Akizungumza katika Wiki ya Sheria kwa Mkoa wa Tanga, Mgumba alisema zipo taarifa za baadhi ya wazazi na walezi wanasuluhisha wenyewe matukio ya ukatili wa kijinsia hali ambayo ni kinyume cha sheria na haki za kibinadamu.

"Tunalaani vitendo vya wazazi na walezi wanaomalizana wenyewe kwa wenyewe na wahalifu wa ukatili kwenye jamii, kwanza hawana mamlaka hayo na ni ukiukwaji wa haki za kibinadamu kisheria pamoja na katiba ya nchi. Suala hili ni kosa la kijinai kama jinai nyingine zozote," alisema.

Aidha, Mgumba ameitaka mahakama kuendelea kutekeleza matakwa ya kikatiba katika kutoa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia haki na sheria. Aliwataka kutojihusisha na uonevu wa aina yoyote katika kutatua migogoro ya wananchi.

"Kwa mujibu wa katiba ibara ya 7(a) inaitaka mahakama kutochelewesha haki bila sababu za msingi, rai yangu kwa mahakama kutekeleza takwa hili la kikatiba tuendelee kumaliza kesi zetu kwa wakati ili kupunguza malalamiko, pia kuendelea kutoa haki bila kujali nafasi ya wahusika katika jamii," alisema.

Meya wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, Abdulrahman Shillow alipongeza mahakama Kanda ya Tanga inavyoendelea kuhudumia wananchi ikiwamo kutatua migogoro mbalimbali na kuwapatia msaada wa kisheria jambo ambalo limepunguza na kuondoa kwa kiasi kikubwa malalamiko katika jamii.

Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Tanga, Beda Nyaki alibainisha kuwa bado jamii ina uelewa mdogo wa masuala ya kisheria.

Wiki ya msaada wa kisheria kwa mwaka huu imebebwa na kaulimbiu isemayo: 'Umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu, wajibu wa mahakama na wadau'.

# Hujuma hifadhini

Na Renatha Msungu, DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema baadhi ya mahakimu, majaji na mawakili wanashiriki kuhujumu maeneo ya hifadhi kwa kupokea rushwa na kuathiri utoaji haki.

Amesema hujuma hizo zinajumuisha mahakama kuzuia minada ya mifugo inayokamatwa kwenye maeneo hayo na kuwatoza faini ndogo wamiliki wa mifugo.

Akizindua Wiki ya Sheria kwenye Viwanja vya Nyerere Square jijini hapo jana, Makamu wa Rais alisema: "Katika ziara zangu ninazofanya mikoani na nyingine zinanikuta ofisini, ninapokea malalamiko mengi ya wananchi kuhusu mhimili wa mahakama lakini na vyombo vingine - polisi na magereza yenyewe, kwenye mfumo wa utendaji na utoaji haki kwa ujumla wake.

"Baadhi ya malalamiko ninayosikia ni kwamba baadhi ya mahakimu, mawakili na majaji sio waaminifu, wanadai rushwa kinyume cha kiapo chao, kuna minada ya mifugo ambayo inakamatwa kwenye maeneo ya hifadhi, mara kadhaa Mbeya kule tunaletewa malalamiko minada hiyo inazuiliwa kwa amri ya mahakama.

"Tena wakati mwingine unashtuka kabisa hiyo mahakama inakaa Jumapili au basi hizo faini ambazo zinaamriwa ni ndogo mno, kwa hiyo mwenye mifugo yake analipa faini baada ya nusu saa anarudisha mifugo yake kwenye hifadhi."

Pia alisema amepokea malalamiko ya fedha za kigeni zinazokamatwa mipakani, zinapotea mikononi mwa mahakama na hukumu zinapindishwa ili kumpa ushindi mwenye fedha.

"Yapo malalamiko mengine, ni pamoja na gharama kubwa za uendeshaji wa kesi na kulipa gharama za mawakili, wananchi wanalalamikia hukumu kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza lakini pia watuhumiwa wanakaa mahabusu muda mrefu wanasubiri uchunguzi kukamilika.

"Wananchi wengine wanasema 'jamani hatuna elimu ya sheria', hivyo kuna ukosefu wa elimu ya sheria kwa umma pamoja na jitihada zote ambazo mmefanya," alisema.

Aliwataka wahusika katika mfumo wa utoaji wa haki kuendelea kutoa elimu kwa umma na kuhakikisha huduma mbadala ya usuluhishi inapatikana na kufikika kwa urahisi.

"Nitoe wito kwa mahakama kushirikiana vyema na wadau katika kuimarisha utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi ili kufikia malengo yake kirahisi," aliagiza.

Makamu wa Rais alisema mawakili wa kujitegemea wanapaswa kujielekeza katika kutoa elimu na ushauri sahihi kwa wateja wao kuhusu namna bora ya kutatua migogoro ikiwa ni pamoja na kutumia njia mbadala ya usuluhishi badala ya kuendelea na kesi mahakamani.

"Asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali yaendelee kutoa elimu kwa umma, misaada kwa wananchi na kujenga uelewa kuhusu haki za msingi za kiraia na umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, pia viongozi wa dini na viongozi wa mila kote nchini wasaidie mahakama kuzungumza na wananchi kuhusu umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi," alielekeza.

Pia aliagiza kuangaliwa upya ufanyaji kazi wa mabaraza ya ardhi nchini kutokana na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi inayokosa usuluhishi wa mapema.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahi[…] Hamis Juma, alitoa rai kwa wananchi wanaohitaji kudai haki zao, kufahamu kwanza haki hizo kwa kusoma na kutafuta elimu itakayowezesha kufahamu sheria na taratibu zinazoongoza haki inayotafutwa.

Alisema Wiki ya Sheria itatumika katika kutoa elimu na kuwakumbusha wananchi namna ya kupata haki zao kwa njia sahihi na rahisi.

Alisema wananchi wana wajibu wa kumaliza mashauri kwa njia ya usuluhishi huku akitoa wito kwa wananchi kutembelea Maonesho ya Wiki ya Sheria na hususani Mahakama Kuu Kituo cha Usuluhishi ili kupata elimu na uelewa zaidi kuhusu njia hiyo iliyosheheni faida lukuki kwa kuwa kufanya hivyo kutawapa nafasi ya kufanya shughuli za uzalishaji na kujiongezea kipato.

"Ni muhimu wananchi wafahamu pia namna ambavyo migogoro ya biashara, kazi au mikataba inayoweza kutokea kwa njia za mitandao," alisema.

Maonyesho hayo yaliyozinduliwa jana yatafanyika kwa siku nane hadi Januari 29 yatajapohitimishwa yakifuatwa na kilele cha Siku ya Sheria itakayofanyika Februari Mosi mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan akiwa mgeni rasmi.


**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI**

**SADICK W. CHIBUGA**

anatangaza kupoteza kadi ya bajaji yenye usajili wa **MC 708DDT.** Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa polisi.

Ametoa taarifa polisi na kupewa namba **IRI/IRI/RB/26552/2023.**



IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE
AT KOROGWE
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.17 OF 2022
IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE BONIFACE MHINA
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATIX
BY ELIZABETH WILLIAM SHEWAI

GENERAL CITATION
(MADE UNDER RULE 75 OF PROBATE RULES ON 369 OF 1963)

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 03 Day of February, 2023.

Date at Korogwe this 19 day of January 2022

# Takukuru kuchunguza tuhuma rushwa kwa majaji, mahakimu

Na Shukuru Mgoba, Mbeya

JAJI Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mustapher Siyani amemuagiza Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Rose Ibrahim awasilishe Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) tuhuma za Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk Rashid Chuachua kuwa kuna majaji na mahakimu wanapokea rushwa kwa njia ya miamala ya simu.

Taarifa ya Mahakama kwa umma ilieleza kuwa Dk Chuachua alitoa tuhuma hizo wakati wa sherehe za uzinduzi wa Wiki ya Sheria mkoani Mbeya.

"Ikithibitika pasipo na shaka kwamba tuhuma hizi zina ushahidi wa kutosha, na bila ya kuathiri hatua nyingine zitakazochukuliwa na vyombo husika, hatua za kinidhamu

zitachukuliwa kwa watumishi hao watakaothibitika kutenda kosa hilo," ilieleza taarifa hiyo na kuongeza:

"Ni matumaini ya uongozi wa mahakama kuwa waliotoa tuhuma watakuwa tayari kuthibitisha ili sheria ichukue mkondo wake bila kumuonea mtu yeyote au kuchafua taswira ya mhimili wa mahakama na watumishi wake."

Dk Chuachua alidai kuwa walipokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi wakidai kuombwa kutoa rushwa kupitia miamala ya simu na walipofuatilia hawakufanikiwa kuzipata namba hizo.

"Mheshimiwa jaji kama nilivyosema wananchi wanakimbilia kwetu na haya nimekusudia leo kuyasema wazi, si rahisi kuwakamata kwa kutumia miamala kwa sababu wakati mwananchi anakuja tayari ameshatoa laki tano, laki sita anakuja kuleta ushahidi wa muamala, sasa fuatilia ile namba ya simu unakuta jina hewa," alisema Dk Chuachua.

Aliongeza: "Hilo lipo ukilitaka nitakuonesha na kazi hiyo tunaifanya, mahakimu wengi wanafanya kazi vizuri lakini hao wachache tunajua mbinu wanazotumia na mie siku ya leo naweza nisiwe mzuri sana kwenye mfumo wa sheria kwenu nyie majaji ambao ni wakubwa, hili tunalitafutia dawa, Takukuru msikie leo wananchi hawa wanataka haki itendeke."

Alivitaka vyombo vya sheria kuanzia Jeshi la Polisi, mfumo wa mahakama, mabaraza ya ardhi kwa kila ngazi kutimiza wajibu kwa kuhakikisha wanasimamia sheria bila kupindisha na kutoa haki kwa wananchi.

Aidha, aliwaomba Takukuru kuangalia suala la ucheleweshaji wa mashauri ya ukatili wa kijinsia vikiwamo vipigo, ulawiti na ubakaji huku akibainisha uwapo wa baadhi ya madaktari wanaopokea rushwa kuharibu ushahidi wa kesi hizo.

"Nitatoa mfano mmoja, yupo mtu wa miaka 70 (umri) alimbaka binti wa miaka 13 katika Kata ya Ilemi, baada ya kupata malalamiko nilienda nyumbani kwao nikakuta ana ujauzito wa miezi saba, nilipofuatilia mwenendo wa kukamilisha ushahidi wa ubakaji nikakuta daktari aliyempokea binti aliandika hana ujauzito, pili aliwashawishi wazazi ujauzito utolewe. Niliagiza Mkurugenzi na Takukuru daktari huyo asimamishwe kazi," alisema Dk Chuachua.

Habari Leo 22/01/2023 uk. 3

# Dk Mpango ataka haki kujenga uchumi



**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU wa Rais, Dk Philip Mpango (pichani) ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango iihusishe Mahakama kikamilifu katika kuandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo inayofuata.

Pia Dk Mpango ameagiza utaratibu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi uimarishwe ili kuepusha visasi huku akitaja kero tisa zinazoukabili mfumo wa utoaji haki nchini.

Alitoa maagizo hayo Dodoma jana wakati akizindua Wiki ya Sheria nchini. Dk Mpango alimtaka Waziri wa Fedha na Mipango, Dk Mwigulu Nchemba na timu yake kuhakikisha wanahusisha muhimili huo kwa ukamilifu katika kuandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo inayofuata baada ya iliyopo kuisha muda wake mwaka 2025.

"Najua Waziri wa Fedha na timu yake wananisikia, timu inayoandaa Dira inayofuata ambayo imekwisha kuundwa lazima ihusishe mhimili wa mahakama kikamilifu. Mheshimiwa Mwigulu alipo bila shaka amenisikia," alisisitiza Dk Mpango.

Alisema Wiki ya Sheria ni muhimu kwa wananchi kupata msaada wa kisheria na kuelewa shughuli za mahakama, hivyo elimu inayotolewa katika wiki hiyo itasaidia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu huduma za mahakama na utaratibu wa sheria kwa ujumla.

Kwa kuwa kaulimbiu ya Wiki ya Sheria mwaka huu inasema 'Umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi katika kukuza uchumi endelevu, wajibu wa mahakama na wadau,' Dk Mpango alisema kaulimbiu hiyo inamkumbusha mambo mawili likiwamo kwamba hakuna uchumi endelevu bila kuwapo haki kwa wananchi na taasisi za kiuchumi.

Alisema haiwezekani kuwa na uchumi endelevu wakati wananchi wanaofanya shughuli za kiuchumi wakiwa hawana haki, hivyo lazima uwepo mfumo thabiti wa kutatua migogoro au kuisuluhisha.

Alitaja jambo la pili kuwa kaulimbiu hii inakumbusha Watanzania kuwa wanaweza kushirikiana na mahakama katika kutatua migogoro baina yao kwa njia ya usuluhishi na kujenga uchumi endelevu wa taifa.

"Usuluhishi unajenga maelewano na mapatano, unawafanya watu kuendelea kushirikiana baada ya kesi kukamilika, ni njia inayoweza kutumika kupunguza mlundikano wa kesi mahakamani na kuepuka gharama kubwa ya kuendesha mashauri ambayo baadhi yake huchukua muda mrefu kukamilika," alisema Dk Mpango.

Alisisitiza "Utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi unaepusha visasi na kuepusha watu kujichukulia sheria mkononi. Naamini migogoro mingi hasa ile ya ardhi na mipaka na ile ya urithi na mirathi inaweza kutatuliwa kwa njia ya usuluhishi na kurejesha amani miongoni mwa wananchi wetu."

Aidha, Dk Mpango aliipongeza mahakama kwa kuandaa sera mpya ya Tehama na kuendelea kuwekeza kwenye matumizi ya tehama katika kutoa huduma kwa kuwa ulimwengu wa sasa umetawaliwa na teknolojia.

Pamoja na mafanikio hayo, alisema bado kuna changamoto ambazo mahakama kwa kushirikiana na vyombo vingine husika haina budi kuzifanyia kazi.

Alizitaja ni pamoja na baadhi ya mahakimu, mawakili na majaji kudai rushwa kinyume cha viapo vyao, fedha za kigeni zinazokamatwa mipakani kupotea mikononi mwa mahakama na wananchi kulalamikia hukumu za mahakama kupindishwa ili kumpa ushindi mwenye fedha.

Alitaja malalamiko mengine ya wananchi kwa mahakama ni gharama kubwa ya uendeshaji wa kesi na kulipa gharama za mawakili, hukumu kuandikwa kwa Kiingereza na watuhumiwa kukaa mahabusu muda mrefu kusubiri uchunguzi ukamilike.

"Wananchi wengine wanasema hawana elimu ya sheria, katika baadhi ya maeneo wanalalamikia umbali mrefu kutoka walipo mpaka mahakamani, wanalalamikia mila na desturi potofu ambazo zinakinzana na sheria hasa kuhusu mirathi na umiliki wa ardhi kwa wanawake na haki za watoto," alisema Dk Mpango.

**Imeandikwa na Matern Kayera (Dar es Salaam) na Sifa Lubasi (Dodoma).**

Uhuru 24/01/2023 uk. 1

**Dk. Mpango ataka majaji, mahakimu kuheshimu viapo**

>>UK. 2

**Rais Dk. Mwinyi aagiza watendaji kutekeleza maagizo kwa wakati**

>>UK. 3

**Dk. Dimwa: Namudu jukumu nililokabidhiwa ndani ya CCM**

>>UK. 15

WIKI YA SHERIA



**MAKAMU** wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiongoza Matembezi ya uzinduzi wa Wiki ya Sheria jijini Dodoma, jana. Wa pili kushoto, ni Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdallah, wa tatu kulia ni Jaji Mkuu wa Tanzania Profesa Ibrahim Juma na kulia ni Mkuu wa mkoa huo, Rosemary Senyamule. **(Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais)**